East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 2, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 2, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Dhima ya Toponemia kama Utambulisho wa Jamii: mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara Nchini Kenya

*Dkt. David Micheni Mutegi, PhD[1*] Dkt. Allan Mugambi, PhD[2] na Dkt. Timothy Kinoti M'Ngaruthi, PhD[3]*

[1] Chuo Kikuu cha Tharaka, S.L.P 193-60215, Marimanti, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P 109-60400, Chuka, Kenya.
[3] Chuo Kikuu cha Embu, S.L.P 6- 60100, Embu, Kenya.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0002-3270-6640; Barua pepe ya mawasiliano: dmisheni@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*21 Novemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Anthroponemia, Dhima, Onomastiki, Toponemia na Uchanganuzi.*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulikuwa wa kionomastiki uliolenga kubainisha dhima ya toponemia za shule za msingi kama utambulisho wa jamii. Utafiti ulifanyika katika eneo la Mwimbi na Muthambi Jimboni dogo la Maara. Nadharia ya Ujinaishaji pamoja na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi na Matini ndizo zilizotumiwa kuongoza utafiti huu. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na hojaji. Mahojiano yalimwezesha mtafiti kupata data ya kutosha na halisi moja kwa moja kutoka kwa wahojiwa. Hojaji ilimwezesha mtafiti kukusanya data kwa urahisi katika maeneo mengi na kutoka kwa sampuli kubwa. Walengwa katika utafiti huu walikuwa wakaazi wa Mwimbi na Muthambi. Usampulishaji ulifanywa kimaksudi kwa kuhusisha machifu 5 wa kata 5 za Mwimbi na Muthambi na manaibu wa chifu 25 kutoka kata ndogo 25 za eneo hili. Watawala hao walichaguliwa kwa sababu wao ni wenyeji wa eneo hili walio na habari kuhusu maeneo yao ya utawala kwa hivyo wangetoa habari kamilifu kuhusu maswali ya utafiti. Sampuli nyingine ya Wazee 20 wenye umri wa miaka sabini na zaidi walichaguliwa kimakusudi kwa kutumia mbinu ya kimtandao ili kutoa habari kuhusu dhima ya toponemia za shule za msingi katika eneo la Mwimbi na Muthambi. Sampuli ya wazee ilipatikana kwa urahisi kwa sababu ndio wanaopata pesa za wazee na walijulikana katika vijiji vyao. Uchambuzi na uwasilishaji wa data ya utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo kulingana na madhumuni na swali la utafiti. Matokeo ya utafiti huu ni marejeleo muhimu kwa watafiti wengine watakaoshughulikia vipengele vya onomastiki katika lahaja ya Kimwimbi na Kimuthambi. Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa toponemia huwa na dhima mbalimbali katika jamii.

**APA CITATION**

Mutegi, D. M., Mugambi, A. & M'Ngaruthi, T. K. (2023). Dhima ya Toponemia kama Utambulisho wa Jamii: mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(2), 1-14. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

**CHICAGO CITATION**

Mutegi, David Micheni, Allan Mugambi and Timothy Kinoti M'Ngaruthi. 2023. "Dhima ya Toponemia kama Utambulisho wa Jamii: mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (2), 1-14. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581.

**HARVARD CITATION**

Mutegi, D. M., Mugambi, A. & M'Ngaruthi, T. K. (2023) "Dhima ya Toponemia kama Utambulisho wa Jamii: mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara Nchini Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), pp. 1-14. doi: 10.37284/jammk.6.2.1581.

**IEEE CITATION**

D. M. Mutegi, A. Mugambi & T. K. M'Ngaruthi "Dhima ya Toponemia kama Utambulisho wa Jamii: mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara Nchini Kenya", *EAJSS*, vol. 6, no. 2, pp. 1-14, Nov. 2023.

**MLA CITATION**

Mutegi, David Micheni, Allan Mugambi & Timothy Kinoti M'Ngaruthi. "Dhima ya Toponemia kama Utambulisho wa Jamii: mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 2, Nov. 2023, pp. 1-14, doi:10.37284/jammk.6.2.1581.

## UTANGULIZI

Onomastiki ni sayansi maalum inayochunguza au kutalii majina hasa ya viumbe. Taaluma hii inajumuisha mbinu za kutambulisha majina ya watu na mahali. Majina ya watu hurejelewa kama anthroponomastiki au anthroponemia katika hali ya ufupisho. Majina ya mahali hurejelewa kama toponomastiki ambalo hufupishwa kama toponemia au topononimia. Taaluma ya onomastiki imegawika katika sehemu mbili kuu ambazo ni anthroponomastiki (majina ya binadamu) na toponomastiki (inayohusiana na majina ya mahali). Toponimia ni aina ya onomastiki inayochunguza majina mbalimbali yanayorejelea mahali au maeneo. Aghlabu binadamu huweza kupata jina la mazingira yake, taasisi, nchi, nyumba na mahali popote pa kijiografia. Sehemu mbalimbali hupata jina kutokana na uasili wake sawa na jamii husika, imani na hata thamani yake (Crystal, 1987).

Rye (2006) na Raybum, (2010) wameshughulikia taaluma ya onomastiki kwa kutumia mkabala wa kiisimujamii. Wataalamu hao walichunguza majina ya mahali na kubainisha mambo mbalimbali ya kiisimujamii yanayosababisha uteuzi wa majina fulani yanayorejelea sehemu mahususi. Aidha, baadhi ya watafiti walizingatia mkabala wa kimofolojia katika kushughulikia taaluma ya onomastiki. Waliangazia vipengele kama vile kubainisha maumbo ya majina ya mahali (Mjapelo, 2009). Walibainisha pia namna majina ya mahali yanavyonyambuliwa ili kuunda majina ya watu waishio katika eneo husika. Rugemalira, (2009) na Buberwa, (2011), walionyesha uamilifu wa viambishi ngeli katika majina ya mahali. Kihore na wenzake, (2004) na Mwendamseke, (2011) walitafiti kuhusu vipengele vya kimofolojia vya nomino za Kibantu kwa kujikita zaidi katika nomino za kawaida pasipo kugusia nomino za pekee zinazotaja mahali. Wataalamu hawa walidai kuwa nomino mahususi huundwa kwa mizizi tu na haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia, madai yaliyoungwa mkono na Karanja, na Habwe, (2007) walioshikilia kuwa nomino za pekee kama vile za mahali hujidhihirisha katika maumbo yake maalum.

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu majina kwa jumla mathalani: Musyimi, (2011) alichunguza maana, ishara maana na misingi ya kitamaduni ya majina ya watu katika jamii ya Wakamba. Aligundua kuwa kulikuwepo na majina mengine kama ya mahali, ya mito na wanyama lakini mipaka ya utafti wake haikumruhusu kuyashughulikia. Hakujishughulisha na majina ya mahali. Masanja, (2019) alifanya utafiti uliohusu uchunguzi wa kisemantiki wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Utafiti wake ulionyesha vigezo vinavyotumiwa katika kuteua majina ya asili na kubainisha miktadha ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu.

Ingawa kipengele cha majina kinaonekana kushughulikiwa na wanaisimu mbalimbali kama ilivyofafanuliwa, utafiti uliofanywa ulishughulikia zaidi semantiki ya majina ya watu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

na mahali na kuepa kushughulikia kwa kina suala la dhima ya toponemia kama utambulisho wa jamii. Ukosefu wa utafiti wa aina hii ulifanya jamii kupungukiwa na maarifa muhimu kuhusu maana na mchango wa toponemia katika utambulishaji wa jamii. Utafiti huu ulilenga kufidia upungufu huu kwa kubainisha dhima ya toponemia za shule za msingi katika jamii za Wamwimbi na Wamuthambi.Swali la utafiti lililojibiwa ili kutimiza madhumuni ya utafiti huu lilikuwa: Toponemia za shule za msingi zina dhima gani katika utambulishaji wa jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi?

## MWAUO WA MAANDISHI

### Umuhimu wa Majina ya Mahali

Majina ya mahali ni mojawapo ya sehemu muhimu ya mazingira ya kijiografia na kitamaduni kama anavyodai Reinsted (1994). Majina huwa yanatambulisha maumbile tofauti ya kijiografia na kuwakilisha amali muhimu za kitamaduni katika fikra za watu. Kulingana naye, majina ya mahali hutuwezesha kuelewa historia ya kijamii ambayo haijarekodiwa na wataalamu wa historia.

Reinsted (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa majina haya yalitolewa na watu wa kawaida waliojibiidisha kuweka kumbukumbu za matukio ya kila siku au shughuli za kazi zilizokuwa uti wa mgongo wa jamii kwa karne nyingi. Mawazo ya mtafiti huyu yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile yalimsaidia mtafiti kuchunguza umuhimu wa toponemia katika utambulishaji wa jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi.

Giles (1979), katika nadharia yake jumuishi anadai kuwa utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea na ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamii lugha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii. Kwa hivyo, majina kama utambulisho wa mtu, kitu au mnyama ni mchakato mmojawapo ambao jamii hutumia ili kuleta utambulisho. Mfano wa kibainishi kinachodumishwa na jamii ni toponemia ambazo hutumiwa kutambulisha maeneo mbalimbali. Maelezo haya yaliufaa utafiti huu kwa vile ulitathmini utambulisho wa jamii kutokana na semantiki ya toponemia. Mojawapo ya maneno ambayo ni vibainishi vya utambulisho yaliyotumiwa katika maelezo ya Giles (keshatajwa) ndiyo pia yaliyotumiwa katika utafiti huu ambayo ni toponemia.

Hog na Abrams (1990) walisema kuwa dhana ya utambulisho wa jamii ni maarifa aliyo nayo mwanajamii kuwa yeye ni wa aina gani kijamii au ni wa kundi gani kijamii. Katika kusisitiza maelezo haya, Banes (2005) anadai kuwa mtu yeyote katika jamii fulani hujitambua kuwa yeye ni wa kikundi fulani kwa kutumia lugha ya jamii hiyo katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Maelezo hayo yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile yalihusiana na dhana ya utamaduni katika jamii suala ambalo pia lilihusiana na utafiti huu uliochunguza namna toponemia za shule za msingi zilivyotambulisha utamaduni wa jamii.

Watu hujitambulisha kwa jina la mahali ambalo liko karibu nao, wanalolifahamu vyema na wanalolimiliki kama asemavyo Thorsten (1994). Anaendelea kueleza kuwa watu hujitambulisha kwa majina ya mahali ya kawaida yanayohusisha jumuiya kubwa. Maelezo ya mtaalamu huyu yalimsaidia mtafiti katika kuchunguza namna toponemia za shule za msingi za eneo la Mwimbi na Muthambi zilivyotambulisha watu wa eneo hili.

Uhifadhi wa majina ya mahali ni rasilmali muhimu na chanzo cha utamaduni ambao ni utambulisho wa watu kama anavyodai Helander (1999). Aidha, majina ya mahali yanaakisi mahusiano ya mwanadamu na maumbile katika vipindi mbalimbali vya wakati ambapo watu waliishi. Sehemu kubwa ya hifadhi ya majina yako katika hatari ya kupotea kutokana na ruwaza za makao na miundo ya maisha ya kiuchumi yanayobadilika kwa kasi. Hali kadhalika, watu walio na habari kuhusu majina ya mahali wanaendelea kutoweka. Maelezo hayo yaliwiana na utafiti huu kwa vile ulidhihirisha umuhimu wa toponemia katika uhifadhi wa utamaduni wa jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

Kulingana na Mbaabu (1996), utamaduni unahusu mila, asili, jadi na desturi ya mavazi, vyakula, imani, tabia na maisha ya jamii kwa jumla. Lugha ni njia maalum ya kuueleza, kuuhifadhi na kuutetea utamaduni wenyewe. Mbaabu, (keshatajwa) anaeleza kuwa lugha na utamaduni wa jamii huhusika katika viwango vyote kama vile tabia, rasilmali, mfumo wa ishara na imani. Maelezo ya mtaalamu huyu yalimsaidia mtafiti katika kufafanua vipengele vya utamaduni kama kitambulisho cha jamii. Aidha, aliweza kubainisha namna toponemia ambazo ni aina ya maneno katika lugha zinavyoitambulisha jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi.

Msanjila (2011) alichunguza na kuonyesha utata uliojitokeza katika ubainishaji wa utambulisho wa msemaji kwa kutumia lugha. Alieleza kuwa utambulisho ni dhana pana kwa maana umebeba mambo mengi ndani yake kama vile: mila, desturi, lugha, historia ya jamii, mavazi, chakula, siasa, imani na uchumi. Haya ni baadhi tu ya vibainishi vya utambulisho wa mzungumzaji fulani kwa kuwa yuko tofauti na mzungumzaji mwingine au jamii fulani iko tofauti na jamii nyingine. Utambulisho wa mzungumzaji ni upekee alio nao mzungumzaji katika kuitumia lugha yake. Hali kadhalika, utambulisho wa jamii ni ule upekee wa jamii unaobainishwa kwa misingi ya kitamaduni ambayo iko tofauti na misingi ya tamaduni za jamii nyingine.

Maelezo haya yaliufaa utafiti huu kwa ambavyo ulihusu utambulisho wa mzungumzaji kwa kutumia lugha na hali kadhalika alifafanua utambulisho wa lugha kwa jamii. Suala hili ni mojawapo ya madhumuni ya utafiti huu ambayo yalibainisha namna toponemia zinavyotambulisha jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi. Hata hivyo, tofauti na maelezo ya Msanjila, utafiti huu haukujihusisha na utambulisho wa mtu binafsi kwa kuzingatia matumizi ya lugha.

Kulingana na Koigi (2008), majina huwa na dhima ya kumtambulisha mtu katika jamii kiutamaduni na hata kiuchumi. Jambo muhimu ni kuwa kila jina huwa na maana maalum iliyo na thamani yake. Ingawa jamii mbalimbali huwa na majina yanayoonekana tofauti kimuundo, kinachodhihirika moja kwa moja ni kuwa jamii hizi mbalimbali huelekea kuwa na mielekeo inayofanana kwa namna mbalimbali ya kupata majina haya. Mawazo haya yalimfaa mtafiti katika kubainisha umuhimu wa toponemia kama utambulisho wa Wamwimbi na Wamuthambi.

Mutembei (2009), alidai kuwa kuna msukumo uliowafanya watu watoe majina kama vile kuwafanya watu wawe na utambulisho wa asili yao, kwa kumtambulisha mtu na eneo analotoka, tabia na sifa zake na kumtofautisha mtu mmoja na mwingine. Hivyo, majina ya mahali ni moja wapo ya maneno yaliyotumiwa na wanajamii katika shughuli zao za maisha ya kila siku. Majina ni miongoni mwa vipengele muhimu sana kwa jamii kwani husaidia kutambulisha utamaduni wao, kueleza asili yao, na maana zinazopatikana katika majina yao. Maelezo hayo ya Mutembei (keshatajwa), yalimsaidia mtafiti kwa sababu alishughulikia mada iliyochunguza majina ya mahali na dhima zake kwa jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi kwa kuchunguza vigezo vya utoaji wa toponemia, maana yake na umuhimu wake katika kutambulisha jamii. Utafiti huu ulipiga hatua zaidi kwa kubainisha miundo mbalimbali ya toponemia katika jamii.

Mukuthuria (2018) anadai kuwa lugha ni muhimu katika kuwatambulisha watu. Utambulisho wa jamii yoyote unaweza kuwa wa kurithishwa au uwe umebadilishwa na kuupanga upya. Maelezo haya ya mtaalamu Mukuthuria (keshatajwa) kuhusu lugha na utambulisho yaliufaa utafiti huu kwa ambavyo yalimsaidia mtafiti kuelewa umuhimu wa majina ya mahali na namna yanavyotambulisha jamii ya Wamwimbi.

## MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ujinaishaji kwa mujibu wa Stuart na Gottlob (2001), na Nadharia ya Uchanganuzi hakiki Usemi na Matini ya Ruth Wodak (2001). Kutokana na nadharia ya ujinaishaji, mtafiti aliweza kubainisha kuwa majina ya mahali yaliakisi dhima mbalimbali katika jamii. Utafiti huu ulibaini kuwa toponemia zilibainisha imani na itikadi za jamii, shughuli za kiuchumi na kitamaduni katika jamii, masuala ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

uongozi katika jamii, kuonyesha hali ya mazingira na maumbile katika jamii na mifumo ya ujinaishaji wa toponemia katika jamii. Nadharia ya Ujinaishaji ina mihimili kama: Mhimili wa mantiki, Mhimili wa ukweli, mhimili wa utamaduni na mhimili wa ufahamu kamilifu wa kitu au mtu. Mihimili ya nadharia hii ilimsaidia mtafiti katika kuchanganua data ya utafiti. Mhimili wa mantiki ulimsaidia mtafiti kugundua mantiki iliyohusu utoaji wa majina ya shule za msingi za Mwimbi na Muthambi. Maelezo yaliyotolewa na baadhi ya wahojiwa na hojaji kuhusu asili na maana ya toponemia hizi yalihitilafiana. Mtafiti alitumia mhimili wa mantiki kuamua maana iliyofaa kutwaliwa kutokana na maana zilizokinzana. Mhimili wa ukweli ulifaa mtafiti katika kubainisha maelezo ya toponemia yaliyofaa kulingana na maelezo yaliyotolewa na wahojiwa na hojaji. Kuna taarifa zilitolewa na Machifu kuhusu toponemia lakini wenyewe hawakuwa na uhakika nazo hivyo ilimbidi mtafiti kupata ukweli kutokana na mahojiano ya wazee.

Utafiti huu uligundua kuwa utoaji wa toponemia ni tukio la kijamii kwa hivyo mhimili wa utamaduni ulifaa katika kuonyesha kuwa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi ziliakisi utamaduni wa jamii. Aidha, mhimili wa ufahamu kamilifu wa kitu au mtu ulikuwa muhimu kwa mtafiti kwani ilimbidi atafute wazee wenye ufahamu wa toponemia kwa sababu si wote waliweza kuzieleza. Katika mahojiano na wazee wakati mwingine mtafiti alielekezwa mahali ambapo angewapata wazee wenye ufahamu kamilifu wa toponemia na wengine waliachwa kwa kuwa hawakuwa na habari ya kutegemewa.

Kwa mujibu wa Wodak (2001), Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi na Matini iliasisiwa na wanaisimu tekelezi katika bara Uropa kama vile Ruth Wodak, Norman Fairclough na Van Dijk. Lengo kuu la nadharia hii ni kuchambua matini kwa kina kwa minajili ya kuleta uangavu zaidi. Nadharia hii ina nguzo tano lakini tatu ndizo zilizotumiwa kuongoza utafiti huu: Mhimili wa Unominishaji au urejeaji, Mhimili wa kubandika majina hasa ya kibaguzi na Mhimili wa kudhihirisha nguvu za usemi.

Mhimili wa Unominishaji au urejeaji: Wodak na Reising (2000), wanadai kuwa nguzo hii huweka wazi namna watu hupewa majina kama njia ya kuwarejelea ili kuwatofautisha na wengine. Unominishaji huu hufanywa kwa njia kadha kama vile kudharaulia mtu kwa tamathali au kubandika majina ya kibaguzi na ya kudhalilisha. Ingawa nguzo hii inahusu namna watu hupewa majina ilisaidia kujibu swali la utafiti lililohusu dhima za toponemia katika jamii. Kwa kutumia nguzo hii mtafiti aliweza kuchanganua majina yanayotumiwa na jamii katika urejeaji wa mahali mbalimbali.

Mhimili wa kubandika majina hasa ya kibaguzi: Fairclough (1995), anaeleza kuwa nguzo hii inahusu muktadha ambapo watu huwabandika wengine sifa na hulka mbalimbali. Watu huwabandika wengine majina kutokana na sifa zao za kimaumbile au kitabia. Sifa hizi zinaweza kuwa nzuri au mbaya. Nguzo hii hudhamiria kufanya matini iwe angavu ambapo mikinzano ya ndani kwa ndani huangaziwa na hasa maswala madogo madogo yaliyogubikwa katika matini huangaziwa. Mhimili huu ulisaidia kuonyesha namna sifa za kimaumbile, kiuchumi na kitabia zilivyochangia utoaji wa toponemia katika jamii. Kwa hivyo, nadharia hii ilikuwa mhimili na dira ya kumulika matendo ya kijamii yaliyoakisi umuhimu wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi.

Utafiti huu ulifaidika kutokana na nguzo hii kwa kujibu swali kuhusu dhima za toponemia katika jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi. Kutokana na nguzo hii mtafiti aliweza kufafanua maana na matumizi ya toponemia mbalimbali za shule za msingi katika jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi.

Mhimili wa kudhihirisha nguvu za usemi: Fairclough. (keshatajwa) anadai kuwa nguzo hii inahusu kujibu maswali yanayohusiana na matamshi katika usemi. Matamshi yanaweza kuwa ya moja kwa moja au yana maana ya ndani. Nguzo hii ilimsaidia mtafiti katika kuchanganua

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

data ya utafiti uliofanywa kwa kuchunguza maana iliyogubikwa katika majina ya mahali ambayo hutumiwa kurejelea sehemu mbalimbali katika jamii ya Wamwimbi ambapo ujinaishaji ni shughuli ya kijamii. Suala la kijamii katika utafiti huu lilikuwa mfumo wa utoaji wa toponemia za shule za msingi katika jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi. Mtafiti kwa hivyo alichunguza maana ya semantiki na pragmatiki za majina ya mahali na namna yalivyotambulisha jamii. Uteuzi wa majina haya ulihusiana na madhumuni na maswali ya utafiti.

## MBINU YA UTAFITI

Utafiti huu ulifanywa katika Jimbo Dogo la Maara Jimboni Tharaka Nithi nchini Kenya. Eneo la Maara linamilikiwa na jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi wenye utamaduni sawa na lahaja zinazokaribiana. Eneo hili lina jumla ya shule za msingi 146 zikiwemo za kibinafsi, za kimisheni na za umma. Mbinu iliyotumiwa katika utafiti huu ni muundo wa kimaelezo ili kubainisha dhima ya Toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi. Muundo huu ulifaa kwa vile uliruhusu matumizi ya mahojiano ya ana kwa ana kama njia ya kukusanya data.

Mtafiti aliteua sampuli kulingana na sifa za kuwa na uwezo wa kutoa data sahihi kulingana na lengo la utafiti huu. Sigh (2007), anasema kuwa, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Utafiti huu ulitumia sampuli ya kimaksudi ambayo iliteuliwa kwa kuchagua aina fulani ya watu ili kuwakilisha makundi maalum katika jamii (Kothari, 2004 na Mugenda na Mugenda, 2008). Watafitiwa 50 walichaguliwa: machifu 5 katoka kata 5 za eneo la Mwimbi na Muthambi, manaibu wa chifu 25 kutoka katika kata ndogo 25 za eneo hili. Sampuli hii ilichaguliwa kwa madhanio kwamba ni wenyeji wa maeneo husika na wangekuwa na ufahamu kuhusu majina ya shule zilizo katika maeneo yao ya utawala. Kwa wale ambao hawakuwa na ufahamu huo ilikuwa nafasi nzuri kwao kuuliza kutokana na wenyeji wa kata zao na hivyo walifanikisha utafiti huu. Mtafiti aliteua sampuli ya wazee 20 wenye umri wa miaka 70 na zaidi kwa kutumia mbinu ya kimtandao. Umri huu ulitiliwa maanani kwa kuwa iliaminika kwamba wazee wana maarifa na tajriba ya kutosha kuhusu maana na dhima ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi. Data katika utafiti huu ilikusanywa kwa njia ya hojaji na mahojiano. Mtafiti alitumia mbinu hizi mchanganyiko kwa lengo la kupata matokeo yaliyo bora kama walivyobainisha Best na Khan (1998) kwamba mbinu moja haitoshelezi katika kupata data zilizoaminika na kukubalika katika utafiti. Uwasilishaji wa data ulikuwa wa kimaelezo ambapo taarifa zilizotokana na hojaji na mahojiano zilifafanuliwa kulingana na maswali na madhumuni ya utafiti.

## MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inahusu uwasilishaji na uchanganuzi wa data iliyokusanywa kutoka nyanjani kwa kutumia mbinu ya hojaji na mahojiano. Uchanganuzi huu wa data ulilenga kubainisha dhima za toponemia katika utambulishaji wa jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi.

### Toponemia Zinazoakisi Dhima ya Mila na Utamaduni wa Jamii

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kutokana na mahojiano na dodoso, toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi ziliakisi mila na utamaduni wa jamii. Mambo yaliyojumuisha utamaduni ni kama vile nyimbo, tohara na ujinaishaji wa watu na mahali.

*Gataniro* ni jina linalotokana na kitenzi *gutana* chenye maana ya kutahiri. Gataniro ni mahali ambapo kitendo cha upashaji tohara kilitendeka. Linatambulisha utamaduni wa Wamwimbi wa upashaji tohara. Kila kijana aliyefikisha umri wa kupashwa tohara ilibidi apitie mviga huu. Upashaji tohara kilikuwa kitendo muhimu kwa jamii kwa sababu kijana alivuka umri wa utoto na kuingia utu uzima, aliheshimiwa na jamii, alipewa majukumu kama kulinda jamii dhidi ya uvamizi,aliweza kurithi mali ya babake na vilevile angeweza kuoa.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

*Kamwangu*: Shule hii ilipewa jina kutokana na wimbo wa kiasili ulioitwa *mwangu.* Jina *Kamwangu* huonyesha kuwa Wamwimbi na Wamuthambi walikuwa na njia mbalimbali za kujistarehesha kama vile nyimbo zilizoimbwa na watu wa rika mbalimbali. *Mwangu* ni wimbo ulioimbwa na vijana waliokuwa kapera na wengine waliokuwa wameoa au kuolewa majuzi. Kulikuwa na nyimbo nyingine kama *Nkururi*, *Mwinjiro na Kirarire*. Aidha Wamwimbi walikuwa wakulima wa mahindi, mtama mawele na ndizi. Hivi ndivyo vyakula vilivyoliwa na vijana hasa kabla ya kwenda kuimba *mwangu.* Kulingana na MhG7, aliyekuwa bi kizee kulikuwa na msemo '*ndathi kwina mwangu ndi mwari ndacoka ndi muka.'* Maana yake ni nimeenda kuimba mwangu nikiwa mwanamwali nikarudi nikiwa mwanamke. Kwa hivyo jina *Kamwangu* linatambulisha utamaduni wa Wamwimbi na Wamuthambi wa kujiburudisha kwa nyimbo za kiasili.

Shule ya msingi ya *Kalewa*. Jina *Lewa* lina maana ya vijana waliotahiriwa. Jina hili linatambulisha Wamwimbi kama jamii ambayo ilithamini mila zao hasa tohara. Walitumia mishale ya *nchege (nungunungu)* katika kutoboa masikio ili kutofautisha waliotahiriwa na wasiotahiriwa. Kulingana na MhM3 (mhojiwa *wa tatu kutoka Muthambi*), jamii ya Wamwimbi hawakula nyama ya baadhi ya wanyama kama *nchege* lakini Wameru wengine kama Wachuka walikula. Jina hili linatambulisha Wamwimbi kama jamii iliyouthamini utamaduni wa tohara. Katika jamii hii vijana ndio waliolinda usalama wa jamii. Kulikuwa na majukumu ya kila jinsia katika jamii hii. Wanaume walilinda usalama nao wanawake walitayarisha vyakula. Aidha, kulikuwa na vikao vya wanaume ambavyo wanawake hawakukubaliwa kuhudhuria.

*Kithitu:* Kwa mujibu wa MhK3(*mhojiwa wa tatu kutoka Kiera*), jina la shule ya msingi ya *Kithitu* huonyesha kuwa Wamwimbi na Wamuthambi walikuwa na utamaduni wa kutunza miti fulani kwa ajili ya utoaji wa kafara. Maeneo yenye miti maalum kama *miuu* haya kulimwa wala kukanyagwa ovyoovyo. Kulikuwa na miiko iliyokataza uharibifu wa misitu kwa nia ya kuhifadhi mazingira. Kwa hivyo jina Kithitu linatambulisha kuwa Wamwimbi walitunza mazingira kwa matumizi maalum kama utoaji wa kafara. Siku hizi miti mingi imekatwa kwa ajili ya kilimo na vilevile kupata makazi ya watu.

Uharibifu huu umesababishwa na ukengeufu wa imani na itikadi ya dini jadi kuhusu mahali maalum pa matambiko.

*Ndumbini:* Maana moja ya *ndumbi* ni kata iliyotiwa nakshi ya manyoya ya kuku na hutumiwa katika nyimbo za kitamaduni. Jina Ndumbini linatambulisha Wamwimbi kama jamii yenye utamaduni wa kutumia maleba yaliyonakishiwa katika uimbaji. Wamwimbi walitambulika kwa nyimbo za kitamaduni kama *Mwangu, Mwinjiro na Kirarire*. Nyimbo hizo ziliimbwa kwa mtindo na mahadhi tofauti tofauti. Jina hili linatambulisha Wamwimbi kuwa wakulima wa mimea kama mawele na mtama. Walipovuna nafaka walizotia vyomboni vilivyotiwa *ndumbi* ili kuongeza nafasi kwa madhumuni ya kutiwa nafaka nyingi. Jina Ndumbini pia hutambulisha utamaduni wa Wamwimbi wa kujenga nyumba za umbo la pia. Siku hizi watu wa eneo hili wanajenga nyumba za kisasa. Shule hii ya msingi ilipewa jina hili kutokana na *ndumbi* zilizotengenezewa mahali hapo.

Jina *Kiriani* linatambulisha Wamwimbi na Wamuthambi kama jamii iliyothamini utamaduni wa tohara. Walikuwa na desturi ya vijana kunyolewa kabisa kabla ya kupashwa tohara. Kitendo hicho kilionyesha kuwa vijana wameacha tabia za utoto na kuanza maisha mapya ya utu uzima. Hii ndiyo sababu walinyolewa kabisa ili nywele mapya zianze kuota wakiwa jandoni. Wakitoka jandoni wangevua tabia za awali na kuwa na hali mpya ya maisha ya utu uzima. Wangepewa jina jipya kuonyesha mwanzo mpya. Aidha, Wamwimbi walikuwa na utamaduni wa kuwanyoa kabisa (*kiria*) mama aliyejifungua. Mtoto aliyezaliwa pia alinyolewa nywele za utoto kisha zikachomwa. Kitendo hicho cha kunyoa nywele kabisa kilionyesha mabadiliko katika maisha ya mama na mtoto. Ilikuwa ni njia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

mojawapo ya kumtakasa mama baada ya kuzaa. Kwa mtoto kitendo hicho kiliashiria mwanzo wa maisha mapya katika ulimwengu wa kujitegemea. Kitendo hicho cha kunyoa nywele kabisa kilichofanyika mahali hapo kilikuwa asili ya jina la shule ya msingi ya Kiriani.

**Shughuli zilizofanywa na Wamwimbi na Wamuthambi**

Taarifa zilizotokana na njia mbili za utafiti ambazo ni mahojiano na hojaji zilibainisha kuwa utoaji wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi uliakisi shughuli zilizofanywa na Wanajamii. Shughuli hizo zingekuwa za kijamii, kiuchumi au za kidini.

*Kiamaogo* ni jina ambalo linatokana na *miugu* ambayo ni aina ya minyaa iliyotumiwa kutengeneza uteo na maghala. Shule hii ilipewa jina kutokana na miti mingi ya *miugu* iliyokuwa mahali hapo. Jina la shule ya msingi ya *Kiamaogo* huonyesha kuwa Wamwimbi walikuwa wakulima wa mimea kama mahindi. Walihifadhi vyakula kwa matumizi ya baadaye. Walihifadhi nafaka kwa kuhangika mtini wakitumia *miungo* (aina ya minyaa) jambo ambalo linadhihirisha kuwa Wamwimbi hawangeibiana vyakula. Wamwimbi pia walitumia vitu vilivyopatikana mazingirani mwao kwa kujiendeleza kiuchumi kama vile kutengeneza uteo na vyumba vya kuku. Wamwimbi walikuwa na roho safi (si wabinafsi) kwa vile walikubali watu kutoka vijiji vingine kupata minyaa ya kuangika mahindi na kutengeneza teo.

*Makuri* ni jina la shule ya msingi iliyo katika sehemu ya Chogoria. Makuri ni aina ya mimea yenye majani yatoayo harufu inayovutia nyuki. Wamwimbi waliyatumia ili *kuota mizinga* (kuyachoma na kuyapaka kwenye mzinga pamoja na mafuta ya kondoo ili kuvutia nyuki). *Makuri* ni jina linaloonyesha kuwa Wamwimbi walikuwa na utamaduni wa kufuga nyuki.

Mimea iliyoitwa *makuri* ilipatikana kwa wingi katika sehemu hii na kwa sababu hii shule ya msingi ilipoanzishwa katika eneo hilo ilipewa jina Makuri.Wamwimbi walitengeneza kileo kutokana na asali waliyorina. Asali pia ilitumiwa katika utoaji wa mahari ambalo ni tukio la kitamaduni kwa Wamwimbi.

*Kajiampau* ni jina la shule ya msingi iliyo katika eneo la Mashariki ya jimbo dogo la Maara linalomilikiwa na Watharaka na Wamwimbi. Asili ya jina hili ni lahaja ya Kimwimbi kwa sababu ndio huita kibuyu *mpau* nao Watharaka hukiita *ndegu.* Jina hili hutambulisha Wamwimbi na Wamuthambi kama jamii iliyopenda kutengeneza uji na kuutia kibuyuni ili uchache. Uji ulitengenezwa na Wanawake kwa kutumia kinu cha kusagia. Wanajamii hawa walitumia uji badala ya kinywaji kama chai ua soda nyakati zote. Uji ulitumiwa katika sherehe na vilevile nyakati za kazi kama kulima na ujenzi.

*Mutiiguru* ni shule ya msingi iliyo katika sehemu ya Muthambi karibu na shule ya upili ya Kajiunduthi. Maana ya jina Mutiiguru ni mti juu katika tafsiri ya moja kwa moja ikiwa na maana ya mti ulio juu. Shule hii ilipewa jina hili kwa sababu mahali ambapo imejengwa paliitwa Muti Iguru kutokana na mti ulioonekana kama uko juu. Mandhari yenyewe ya mahali hapa huonekana kwa mbali kuwa juu kwa sababu ya kilima na ardhi tambarare inayofuata. *Mutiiguru* ni jina la shule ya msingi linaloonyesha kuwa Wamwimbi na Wamuthambi walikuwa na mfumo wa utoaji majina ya mahali kulingana na vitu vilivyoonekana mahali fulani kama vile miti, mito, vilima na mabonde. Aidha, Wamwimbi na Wamuthambi walikuwa na mpango maalum wa kujilinda kutokana na maadui kama vile kuwa na ngome ambamo wazee na vijana walikaa. Walijenga vyumba juu ya mti ili kuhakikisha usalama kwa sababu wangeona maadui kwa mbali na kuwashambulia.

*Gianchuku* ni shule ya msingi iliyo katika nyanda za juu za kata ya Chogoria. Jina *nchuku* linamaanisha ghala la kuhifadhia nafaka. Shule hii ya msingi ilipewa jina hili kwa vile kulikuwa na maghala mengi katika sehemu hii. Jina *Gianchuku* linaonyesha kuwa Wamwimbi walikuwa wakulima wa nafaka kwani ndizo zilizohifadhiwa ghalani. Walihifadhi nafaka zao katika maghala ili watumie kwa muda mrefu. Kuwepo kwa *nchuku*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

(maghala) kunaonyesha kuwa jamii za Wamwimbi na Wamuthambi zilijitosheleza kwa chakula.

*Mbironi ni* shule iliyo katika kata ya Ganga. *Mbiro* ni masizi yanayosalia baada yakitu fulani kuteketezwa. Shule hii ilipewa jina hili kwa sababu mahali ilipo palikuwa na masizi mengi kutokana na miti yenye miiba iliyochomwa kwa ajili ya kilimo. Jina la shule ya msingi ya Mbironi huonyesha kuwa Wamwimbi na Wamuthambi walikuwa wakulima kwa sababu walichoma vichaka na miti ili kutayarisha mashamba kwa kilimo. Kulikuwa na kazi ya wanaume na ya wanawake. Wanaume walifyeka vichaka na kazi nyingine zilizokuwa ngumu na hatari kama kukata miti yenye miiba, kufukuza wanyama hatari na kuchoma vichaka nao wanawake wakatengewa kazi iliyokuwa rahisi kama kupika na kutunza watoto.

*Kangethia* ni shule iliyo katika sehemu ya Muthambi. Jina la shule hii limetokana na kitenzi *kungethia*. Maana ya *kungethia* ni kukaa ange au kuzubaa. Kutokana na habari kuhusu asili ya jina hili la shule ya msingi ya Kangethia inabainika kuwa Wamwimbi na Wamuthambi walikuwa wakulima. Walikuza mimea ya vyakula na vilevile wakakuza kahawa kwa ajili ya mauzo. Inadhihirika pia Wamwimbi hawakutaka kulipa ushuru kwa serikali ya kikoloni. Walihisi kuwa wanasurutishwa kutoa ushuru ambao haukuwafaidi kama jamii ila wachache walioshirikiana na Wakoloni. Kulingana na MhM 16 (*mhojiwa wa kumi na sita kutoka Muthambi*), wafanyi kazi wa kiwanda cha kahawa walikataa kuwapimia wakulima kahawa yao kwa vile hawakutoa ushuru. Kahawa ilishinda siku nzima ikiwa guniani kitendo kilichorejelewa na Wamwimbi na Wamuthambi kama *kungethia.* Tangu siku hiyo mahali hapo palijulikana kama *Kangethia.*

**Toponemia Zinazotambulisha Itikadi na Imani za Jamii**

Mojawapo ya dhima ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi ilikuwa ni kuonyesha imani na itikadi za watu kuhusu masuala mbalimbali ya jamii. Masuala kama vile imani kuhusu nguvu za Kiungu na pepo wabaya waliosumbua watu na kusababisha utoaji wa kafara na matambiko kama njia ya kupambana nao.

*Kauni* ni jina la shule ya msingi ambayo iko katika kata ya ganga. Ilipewa jina hili kutokana na miti ya *miuu* iliyokuwa katika sehemu hiyo. Miti hii ilikuwa na matumizi maalum hasa pale ambapo kafara ilitolewa. Jina la shule ya msingi ya *Kauni* linaonyesha kuwa eneo la Mwimbi lilikuwa na miti ya kiasili iliyotunzwa ili kuhifadhi mazingira. Wamwimbi walitoa kafara katika mahali maalum kama vile kwenye misitu au miti iliyohifadhiwa. Kwa hivyo, Wamwimbi walikuwa na itikadi kuwa mahali penye miti maalum walipotolea kafara na matambiko hapangechezewa kwa kukata miti au kupakanyaga ovyo ovyo.

Shule ya msingi ya *Igakiramba* iko katika eneo la Kiera linalokabili mlima Kiera. Jina hili lilitokana na mti ulioitwa *Muramba* au Mbuyu kwa Kiswahili. Jina *Igakiramba* linatambulisha mfumo wa kutoa majina ya mahali uliotumia kigezo cha kitu kilichopatikana mahali fulani. Jina hili ladhihirisha kuwa kulikuwa na miti ya kiasili katika sehemu ya Mwimbi ambayo iliaminiwa kuwa muhimu katika utekelezaji wa majukumu kama vile matambiko. Walikuwa na itikadi kuwa miti hiyo haikustahili kukatwa wala kuchezewa. Mahali ilipokuwa palitunzwa na kuheshimiwa.

*Kagira* ni jina la shule ya msingi iliyo katika eneo la Ganga. Jina la shule hii lilitokana na kitenzi *kugira* kinachomaanisha kuzuia au kukataza jambo kwa kuwa ni mwiko. Shule ya Kagira ilipewa jina hili kutokana na imani kuwa mahali hapo palikuwa pametengwa na kuzuiwa kukanyagwa na watu kwa sababu ya nguvu zisizo za kawaida zilizokuwapo. Jina *Kagira* linatambulisha Wamwimbi kuwa watu waliokuwa na itikadi na miiko iliyowazuia kufanya baadhi ya mambo kama vile kukata miti katika sehemu fulani. Waliamini uwepo wa majini ambayo yalihusishwa na itikadi fulani. Wamwimbi waliogopa mahali palipowekewa vizuizi vya kutoenda mahali hapo au kupachezea. Waliamini kuwa yeyote angekiuka miiko fulani angepatwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

na maafa ambayo yangemwathiri yeye na na labda jamii yake.

*Gituntu* ni shule ya msingi ambayo inapatikana katika sehemu ya Muthambi mahali panapopakana na kata ya Chogoria. Jina hili linatokana na mti ulioitwa *mutuntu* ambao majani yake huliwa na mbuzi. Shule hii ilipewa jina hili kutokana na *mutuntu* uliokuwa mahali ambapo shule hiyo ilijengwa. Jina Gituntu linakumbusha jamii ya Wamwimbi kuwa walivamiwa na maradhi ya matubwitubwi (mumps). Kabla ya ugunduzi wa dawa za kemikali za kuutibu. Wamwimbi walikuwa na itikadi kwamba baadhi ya maradhi yangeweza kuponywa kupitia vitendo kama kuzunguka miti fulani. Hii ndiyo sababu walizunguka *mutuntu* wakiimba, '*Mutuntu ngwatia gukamata mutuntunkai' (*kumaanisha mutuntu nisaidie kuondoa ugonjwa wa matubwitubwi) ili kupata uponyaji.

**Dhana ya Asili na Matukio ya Kihistoria ya Jamii**

Toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi zina dhima ya kutambulisha asili na matukio ya kihistoria ya jamii. Baadhi ya matukio yalikuwa mema ilhali mengine yalikuwa mabaya kama vile kuvamiwa na maadui au matukio ya kimaumbile yasiyosababishwa na binadamu kama vile matetemeko ya ardhi na gharika.

*Kanyambo* ni la kituo cha kibiashara kilicho karibu na shule ya upili ya Igwanjau. Katika eneo hili la Kanyambo kulikuwa na shule iliyoitwa *Great Minds*. Jina Kanyambo linatokana na *nyambo* (vijiti vilivyochongwa) na kushindiliwa mtaroni uliozingira kambi ya wakoloni kwa ajili ya ulinzi dhidi ya Maumau. Inabainika kuwa Wamwimbi walitumia matawi yenye miiba ili kuzingira maboma ya mifugo. Huu ndio mfano ulioigwa na Wakoloni kwa kutumia nyambo kuzingira kambi yao. Licha ya kujikinga kwa jinsi hiyo, Wakoloni walitimuliwa na Waafrika waliodhaniwa kuwa na akili duni kuwaliko.

*Kabaikubu* ni jina la shule ambayo iko katika sehemu ya Kiera kando ya Mlima Kiera. Asili ya jina Kabaikubu ni kitenzi *gukububanua* kwa maana ya kupiganishwa. Shule hii ilipewa jina hili kwa sababu watu wa sehemu hii walihisi kuwa waliteswa na watu kutoka sehemu ya Igoji walipofika sehemu hii. *Kabaikubu* ni jina la shule ya msingi linalotambulisha Wamwimbi kama jamii mojawapo ya Wabantu waliofika eneo hili kutoka *mbwaa* (pwani ya Kenya). Linadhihirisha kuwa uhusiano wao na kabila jirani katika sehemu hii haukuwa mwema kwani walipigana ili kunyanganyana mashamba na mifugo. Inabainika kuwa Wamwimbi walitumia mtindo wa kuwapa watu majina kwa kuzingatia tabia ya mtu. Hii ndiyo sababu kulikuwa na mtu aliyeitwa Baikubu kutokana na kitendo cha kusukumana baina ya makundi mawili.

**Hali na Mazingira ya Mwimbi na Muthambi**

Toponemia nyingine za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi zilisawiri mazingira na mwonekano wa sehemu mbalimbali. Hali hii huwa ya kimaumbile au iliyosababishwa na shughuli za mwanadamu. Watu walio katika maeneo yenye hali ambazo ni tisho kwa maisha yao huzua mbinu za kupambana na hali hizo ili kujiendeleza kimaisha.

*Uthaini* ni shule ya msingi ambayo iko katika kata ya Ganga mkabala wa mlima Kiera. Jina hili linatokana na *Uthai* ambayo ni nomino ya dhahania inayomaanisha hali ya ukosefu wa rutuba katika udongo hivyo, kutoweza kuzalisha mimea na kutofaa kwa kilimo. Jina la shule ya msingi ya *Uthaini* linaonyesha kuwa japo eneo la Mwimbi lilijulikana kwa kilimo, kuna sehemu ambazo ni kame sana. Kuna maeneo ambayo hayakuzi mimea ya vyakula bali hutegemea maeneo mengine kwa chakula. Jina hili linatambulisha Wamwimbi kuwa watu wenye bidii na hutumia rasilimali walizo nazo ili kujikimu. Hii ni kwa sababu japo eneo la *Uthaini* ni kame wanafuga wanyama kama mbuzi na ng'ombe kwa ajili ya mapato yao.

*Ntakani* ni shule ambayo iko katika eneo la Muthambi katika kata ya Kandungu. Jina *Ntaka* humaanisha matope. Kwa hivyo shule hii ilipewa jina hili kwa sababu kulikuwa na matope mengi yaliyonata na kutatiza usafiri katika sehemu hiyo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

Jina hili linatambulisha kuwa sehemu fulani za Muthambi zina udongo tofauti na nyingine. Kuna maeneo ambayo hata kukinyesha shughuli za usafiri hazitatizwi ilhali nyingine hazipitiki. Eneo hili la Muthambi huwa na matope yanayonata kiasi cha kukwamiza usafiri hali ambayo ni chanzo cha ukosefu wa maendeleo katika sehemu hii ya Muthambi.

Shule ya msingi ya *Kiera* iko katika kata ya Kiera kwenye barabara kuu itokayo Keria hadi Kathwana ambapo ni makao makuu ya jimbo la Tharaka Nithi. Jina la shule hii limetokana na jina *Ira* linalomaanisha chokaa. Mwasisi wa shule hii ya msingi aliipa jina Kiera kutokana na umaarufu wa mlima Kiera ulio wa pekee katika eneo la Mwimbi. Kwa jina lingine mlima huu huitwa *Kirima kia Mwimbi*, yaani Mlima wa Mwimbi. Kwa sababu hii Wamwimbi walitambulishwa na mlima huu wenye jina Kiera au mlima wa Mwimbi. Walipenda kujipamba kwa kutumia chokaa na *nondo* (waja) zilizopatikana katika mlima Kiera.Walijipamba wakati wa kuimba nyimbo za kitamaduni na katika sherehe mbalimbali mathalani za tohara. Jina hili pia linawatambulisha Wamwimbi kama watu waliokuwa na utamaduni wa utoaji kafara katika mahali teule kama mlimani Kiera.

Shule ya msingi ya *Makengi* iko katika kata ya Kiera upande wa kusini wa mlima Kiera. *Makengi* ni vitu vilivyotoka ardhini mfano wa vigae vilivyometameta. Shule hii iliitwa Makengi kwa sababu ya *makengi* yaliyotoka kwenye mlima huu ulio karibu na shule. Jina la shule hii linaonyesha kuwa jamii ya Mwimbi ilitoa jina la mahali kulingana na kitu kilichopatikana mahali fulani. Kuwepo kwa *makengi* katika eneo hili ni dhihirisho la uwezekano wa kuwa na madini fulani katika mlima Kiera. Eneo hili vilevile lilivutia Wazungu kwa sababu walitarajia kupata madini katika sehemu hiyo. Wamwimbi walitumia vumbi jeupe (chokaa) iliyotoka kwenye sehemu zilizochimbwa katika kupaka nyumba zao ili zipendeze.

*Ndintune* ni jina la shule ya msingi ambayo inapatikana katika sehemu ya Kiera upande wa Kaskazini mashariki mwa mlima Kiera. Maana ya *Ndintune* ni ardhi au nchi nyekundu. Kulingana na MhK 1(*mhojiwa wa kwanza kutoka Kiera*), udongo ulio katika sehemu ambayo shule hii imejengwa ni mwekundu jambo ambalo lilichangia utoaji wa jina la shule hii. Kutokana na jina hili, inabainika kuwa Wamwimbi walikuwa na mfumo maalum wa kutoa majina ya mahali kwa kutumia sifa za mwonekano wa mahali.

**Dhana ya Utabaka na Utangamano katika Jamii**

Dhima nyingine ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi inahusu dhana ya utabaka na utangamano katika jamii. Toponemia hizi zinaonyesha namna wanajamii walivyohusiana na kutegemeana katika harakati za maisha.

Shule ya msingi ya *Wiru* inapatikana katika sehemu ya Chogoria karibu na barabara kuu itokayo Chuka kuelekea mjini Meru. Nomino hii imetokana na kivumishi *mukeru* kinachofafanua nomino *Nkia*. *Nkia* ni maskini na *mukeru* ni asiye na chochote. Maneno haya hutumiwa kama *Nkia mukeru* kumaanisha maskini asiye na kitu. Shule hii ilipewa jina hili kwa vile watu wa sehemu hii walibaki maskini hohe hahe baada ya kutengwa na utawala wa wakati huo. Jina *Wiru* linadhihirisha kuwa Wamwimbi walikuwa na viongozi waliotegemewa katika maendeleo ya jamii. Iwapo kiongozi hangeunga mkono shughuli za maendeleo katika jamii watu wa jamii wangekuwa maskini hohe hahe. Hali hii ilitokea katika eneo la Wiru ambapo watu walibakia kuwa maskini baada ya kutoungwa mkono na Chifu Mbogori aliyetawala eneo zima la Mwimbi.

*Chogoria* ni jina linalotumiwa katika kurejelea shule za msingi za malazi katika eneo la Chogoria. Jina *Chogoria* linatambulisha Wamwimbi kama watu waliowakaribisha wageni kama vile Wazungu katika eneo lao. Wengi walithamini maendeleo yaliyoletwa na Wakoloni kama vile huduma za afya na masomo. Waliathiriana na Wakoloni katika hali ya maisha. Kwa mfano, walipokea elimu ya kigeni nao wageni wakajifunza baadhi ya maneno ya Kimwimbi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

kama vile *kunyogoria mauntu* ambalo ndilo jina asili la Chogoria.

**Utambulisho wa Watu Mashuhuri katika Jamii**

Kuna toponemia ambazo hutokana na majina ya watu mashuhuri katika jamii. Watu hao wanaweza kuwa walioongoza jamii au waliotenda matukio makuu katika jamii kama vile kuanzisha miradi fulani ya maendeleo. Maelezo haya yanashadidiwa na utafiti wa (Kirui, 2016) aliyebainisha kuwa majina ya watu mashuhuri yalichangia utoaji wa toponimi za Wakipsigisi wa Bometi.

*Murunga* ni shule ya msingi ambayo iko katika kata ya Ganga karibu na kituo cha kibiashara cha Mukui. Shule hii ilipewa jina kutokana na mtu aliyeitwa Murunga. Jina la shule hii linatambulisha kuwa Wamwimbi waliungana kulinda raia na mifugo au mali yao dhidi ya uvamizi kutoka kwa makabila mengine kama Waimenti. Aidha, Wamwimbi walikuwa na misemo iliyojulikana nao tu kwa mfano, '*nibwiji mainya ma Murunga?'* Mnajua uwezo wa Murunga? Maneno hayo yalisemwa na Murunga alipombana kwa mkono mmoja adui mmoja na kuwaita wenzake wamsaidie.

Shule ya msingi ya *Mwimbi* iko katika eneo la Chogoria. Ni shule ya malazi ya umma ambayo ni maarufu sana katika matokeo ya mtihani wa Kitaifa wa KCSE. Shule hii ilipewa jina hili ili kujinasibisha na kiongozi shupavu aliyewaongoza Wamwimbi kutoka *mbwaa* ambapo palikuwa mahali pao pa chimbuko. Jina la shule ya msingi ya *Mwimbi* linatambulisha asili ya Wamwimbi kuwa ni pwani ya Kenya mahali palipoitwa *Mbwaa*. Kulingana na MhK 1(*mhojiwa wa kwanza kutoka Kiera)* na MhK3 (mhojiwa wa tatu kutoka Kiera), eneo hili la Mwimbi lilipata jina kutokana na kiongozi aliyeitwa Mwimbi ambaye aliwaongoza Wamwimbi kutoka pwani ya Kenya. Kutokana na jina hili ni wazi kuwa Wamwimbi waliweza kujitegemea kiuongozi na kwa vyakula katika eneo lao.

**Suala la Elimu katika Jamii**

Baadhi ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi zilitokana na mawazo ya kuimarisha viwango vya elimu miongoni mwa jamii. Shule hizo zilianzishwa na watu binafsi au Misheni mbalimbali. Shule nyingi katika kategoria hii zimetambuliwa kwa majina ya watu wa dini kama vile watakatifu fulani kwa upande wa dini ya Katoleki lakini bado zinahusisha majina ya asili ya mahali zilipojengwa.

*Gateway* ni jina la shule ya msingi ya malazi iliyo katika mji wa Chogoria. Maana ya jina la shule hii ni lango la kupitia. Jina la shule ya msingi ya *Gateway* linatambulisha kuwa miongoni mwa Wamwimbi wapo walioathiriwa na mawazo ya Kikoloni. Kuna baadhi ya Wamwimbi wanaodhani kuwa lugha ya Kimombo huwasilisha dhana vyema kuliko lugha ya Kimwimbi. Mwasisi wa shule hii alichagua jina hili kwa madhanio kuwa Wamwimbi walithamini elimu kama nguzo ya kuimarisha maisha yao na kama urithi wa pekee ambao mzazi angemwachia mwanaye.

*Translight academy* ni shule ya msingi iliyo katika eneo la Chogoria. Maana ya jina hili ni kupitisha mwangaza. Mwasisi wa shule hii alikusudia kuwa shule hiyo ingepitisha mwanga wa elimu kwa watu. Hili ni jina linalovutia kwa sababu linahusu upitishaji wa elimu kwa watu. kimuundo jina hili limehusisha kitenzi na nomino. Neno *Trans* kwa kirefu ni *transfer* linalomaanisha kuhamisha, nalo *light* ni nomino inayomaanisha mwangaza. Kwa hivyo majina mawili yameungana kuunda jina *translight* linalomaanisha kupitisha mwangaza. Kwa sababu hii watu wanaelewa kuwa hii ni shule ambayo wanaojiunga nayo hupata mwangaza wa elimu. Jina hili lina mvuto kwa umma wanaopenda elimu. Jina translight lina dhima ya kuonyesha umuhimu wa elimu kwa hivyo jamii ya Mwimbi ilithamini masomo kutokana na shule nyingi zilizo na majina yavutiayo watu kupata elimu.

*Little Friends* ni shule ambayo iko katika kata ya Chogoria. Ni shule ya chekechea ambayo inahusika tu na watoto wadogo. *Little friends* ni

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

marafiki wadogo au wachanga. Jina hili linavutia kwa sababu hakuna mtu asiyependa rafiki wa watu. Kwa hivyo, jina hili linamaanisha kuwa hii ni shule ya marafiki. Waliojiunga na shule hii huwa marafiki na walihusiana vyema. Kimuundo jina hili limehusisha kivumishi na nomino ambao ni mtindo unaokubalika katika lugha ya Kiingereza. Katika Kiswahili muundo huu haukubaliki. Muundo sawa ni nomino halafu kivumishi kwa hivyo likitafsiriwa kwa Kiswahili jina la shule hii lingekuwa *shule ya marafiki wachanga* badala ya *wachanga marafiki shule*. Kwa hivyo mchakato uliotumiwa kuunda jina la shule hii ni nomino na kivumishi. Dhima ya jina hili ni kuonyesha jamii ya Wamwimbi ilithamini uhusiano mwema na watu wengine. Hii ndio sababu shule inapewa jina la marafiki wachanga ili kukuza hisia za urafiki katika akili za watoto wachanga kwa madhumuni kuwa wangedumisha hali hiyo wakiwa wakubwa.

*Victors' academy* ni shule ya msingi iliyo katika kata ya Kiera kwenye barabara kuu ya kutoka Keria hadi Kathwana. Ni shule ya kibinafsi. Maana ya *victors* ni mabingwa. Ubingwa unaorejelewa ni wa masomo wala si wa mambo mengine. Jina hili linavutia watu wote wapendao masomo kwani humaanisha kuwa mwanafunzi yeyote ambaye angejiunga na shule hii angefaulu masomoni. Mchakato uliotumiwa kuunda jina hili ni nomino na kivumishi. Jina *Victors* linamaanisha mabingwa wa nasomo. Kwa hivyo kulingana na muktadha huu waliojiunga na shule hii hufaulu katika masomo. Jina hili limetumika kuvutia watu ili wapeleke watoto wao katika shule hii. Dhima ya jina hili ni kuonyesha umuhimu wa elimu. Wamwimbi hawakuchagua shule za watoto wao vivi hivi ila walichunguza matokeo ya shule hizo katika mitihani ya kitaifa.

*Great minds academy* ni shule ya msingi iliyo katika kata ya Ganga katika kituo cha kibiashara cha Kanyambo. Ni shule ya kibinafsi. *Greatminds* humaanisha mawazo makuu katika tafsiri ya moja kwa moja. Maana halisi iliyokusudiwa na mdhamini wa shule hii ni shule ya wanafunzi wenye hekima ya juu. Jina hili lina maana kwamba wanafunzi wanaosomea katika shule hii wanapata hekima kuu kutokana na walimu walio na hekima kuu. Muundo wa jina hili ni kivumishi na na nomino. Huu ni muundo unaotumiwa katika lugha ya Kiingereza lakini katika Kiswahili sanifu muundo huu si sawa. Katika Kiswahili nomino hufuatwa na kivumishi bali si kivumishi halafu nomino. Hii ni kwa sababu kivumishi hufafanua nomino au kiwakilishi chake. Dhima ya jina hili ni kuonyesha kuwa wakaazi wa Mwimbi walithamini masomo. Hii ndiyo sababu baadhi ya majina ya shule za msingi hasa za kibinafsi yaliyotolewa kutokana na majina yavutiayo kuhusiana na masomo.

## HITIMISHO

Utafiti huu ulibainisha dhima ya toponemia za shule za msingi katika utambulishaji wa jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi. Mtafiti aliongozwa na lengo mahsusi na swali la utafiti. Matokeo yalionyesha umuhimu wa toponemia kama vile kutambulisha shughuli zilizofanywa katika jamii, imani na itikadi za jamii, mazingira na maumbile katika jamii na suala la elimu katika jamii.

## ORODHA YA VIFUPISHO

MhC: Mhojiwa kutoka sehemu ya Chogoria

MhG: Mhojiwa kutoka sehemu ya Ganga

MhK: Mhojiwa kutoka sehemu ya Kiera

MhM: Mhojiwa kutoka sehemu ya Muthambi

## MAREJELEO

Abrams, D. na Hog, M. (1990). An introduction to the social identity Approach, University of Melbourne, Austrilia.

Barnes, H. (2005). 'Hidasta personal names': *An Interpretation Plains Anthropologistics.* Journal of anthropological Research /25 90311-31281.

Best, J, &Khan, J. (1998). *Research in Education*, New Jersey, Eaglewood Cliffs.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1581

Buberwa, A. (2011). Viambishi ngeli katika nomino za pekee: mifano katika majina ya Kihaya, Kiswahili, Juz. 74. Kur. 41 – 48

Crystal, D. (1987). The Encyclopedia of Language. Cambridge: CUP.

Giles, H. (2001). "Speech accommodation" in R. Methrie (ed) Concise Encyclopedia of Socialinguistics 193-197, Elsevier.

Helander, K. (1999). Place names in multilingual areas in Norway. *Journal of anthropological Research* /25 90311-312

Habwe, J., &Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Kihore, P., & Wenzake, (2004). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu:* Sekondari na Vyuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Kirui, R. (2016). *A morphosemantic study of Kipsigis toponyms.* (Unpublished) Master thesis.Kenyatta University.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kothari, C. (2009). *Research Methodology*: *Methods and Techniques*, New Delhi: New Age International (P) Ltd. 189.

Koigi, K. (2008). Lugha kama Kitambulisho. Jarida la Kiswahili la Isimu na Fasihi. Juz na. 4:23, TUKI, Dar es Salaam.

Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa*, Educational Researchand Publication. Nairobi: Publisher.

Masanja, N. (2019). Uchunguzi wa kisemantiki wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu.Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Msanjila, P., & Wenzake, (2011). Isimujamii, *Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam : TUKI.

Majapelo, P. (2009). Namna ngeli zinavyosaidia kuunda majina ya watu (unpublished) M.A Dissertation. University of Dar-es-salaam.

Mugenda, M., &Mugenda, G. (2008). Research Methods: qualitative and quantitative approach.Nairobi Acts press.

Mukuthuria, M. (2018). "Uchanganuzi wa Lugha za Kibantu za Kenya Katika Ngazi ya Mofolojia: Mtazamo wa Sarufi Zalishi Geuza Umbo." Katika*: Islamic University Journal, Vol. 1 No.2, Mbale – Uganda (uk. 103 – 108).*

Musymi, D. (2011). Maana za majina ya Watu katika jamii ya Wakamba, Tasnifu ya shahada Ya uzamili, Kenyatta University *Bantu Names.* Kiswahili (61):28-49. 190 New Age International Publishers. Ltd

Mwenamseke, F. (2011). *Uainishaji wa ngeli katika lugha ya Kibena.* Tasnifu ya Uzamili (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Raybum, A. (2010). *Place names.* The Canadian Encyclopedia- Historical- Dominion

Reinsted, A. (1994). *Place names of New Zealand* Wellington A. H .& A.W Reed.

Rye, J. (2006). *A popular Guide to Norfolk Place names.* Guist Bottom: Larks Press.

Rugemalira, J. (2009). *A Grammar of Runyambo*, Dar es Salaam: Language of Tanzania Project, University of Dar es salaam.

Sigh, K. (2007), *Qualitative Social Reseach Methods*, Indian: SAGE Publication.

Stuart, M. na wenzake, (2001). *Different types of dictionaries* Grin Verlang.

Thorsten, A. (1994). *Place names worthy of caring for.* Paper read at the symposium place name culture organized by the National Heritage board. Stockholm.

Wodak, R. (2001). *Methods of critical Discourse analysis*,London Sage Publisher.